

MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) litafikisha **Miaka 50** mwezi Novemba 2023 tangu kuanzishwa kwake. Katika kuadhimisha **Miaka 50** Baraza linatarajia kufanya yafuatayo:

- (a) Kupanda miti katika shule za msingi na sekondari nchi nzima. Zoezi hilo lilianza mwezi Oktoba na linatarajia kukamilika mwezi Desemba 2023.
- (b) Kuendesha mafunzo kwa walimu wa Taaluma kuhusu Utunzi wa maswali yanayopima umahiri na mada zenye changamoto ya ujifunzaji. Baraza liliendesha mafunzo kuanzia tarehe **9 Novemba 2023** hadi tarehe **10 Novemba, 2023** kwa walimu wa Taaluma **180** wa shule za msingi na sekondari. Walimu hao waliteuliwa katika Halmashauri za Mkoa wa Tanga.
- (c) Kutakuwa na Kongamano la Kitaaluma litakalofanyika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuanzia tarehe **27 Novemba, 2023** hadi tarehe **28 Novemba, 2023**.
- (d) Uandishi wa Kitabu cha Historia ya Baraza la Mitihani la Tanzania (1973-2023)
- (e) Maonesho ya kazi za Baraza la Mitihani la Tanzania na Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Maonesho hayo yatafanyika kuanzia tarehe **30 Novemba, 2023** hadi tarehe **3 Desemba, 2023**.
- (f) Ujenzi wa Mnara wa Makumbusho utakaozinduliwa tarehe **4 Desemba, 2023**.
- (g) Kilele cha Maadhimisho kitakachofanyika tarehe **4 Desemba, 2023** katika Ofisi za Baraza la Mitihani, Dar es Salaam.